



Hapo zamani za kale,  
wasichana watatu  
walienda kutafuta  
kuni.



Ilikuwa siku yenye joto  
kwa hivyo walienda  
mtoni kuogelea.  
Walicheza  
wakirushiania maji na  
kuogelea.



Ghafla, waligundua  
kuwa saa zilikuwa  
zimeenda.  
Waliharakisha kurudi  
kijijini.



Walipokuwa karibu nyumbani, Nozibele aliweka mkono wake shingoni. Alikuwa amesahau mkufu wake! "Tafadhali rudini nami!" aliwasihii marafiki zake. Lakini, marafiki zake walisema kwamba saa zilikuwa zimeenda sana.



Kwa hivyo Nozibele  
alirudi mtoni  
pekeyake. Aliupata  
mkufu wake  
nakuharakisha kurudi  
nyumbani. Lakini,  
alipotea gizani.



Kwa umbali aliona  
mwangaza ukitokezea  
chumbani.  
Aliharakisha kuelekea  
chumba hicho na  
kubisha hodi  
mlangoni.



La kushangaza ni kuwa mbwa ndiye aliufungua mlango na kusema, "Unataka nini?" "Nimepotea, nahitaji mahali pa kulala," Nozibele alisema. "Ingia ndani, au nikuume!" mbwa akajibu. Nozibele aliingia.



Kisha mbwa akasema,  
“Nipikie chakula!”  
“Lakini sijawahi  
kumpikia mbwa  
chakula,” Nozibele  
aljibu. “Pika, au  
nikuume!” mbwa  
akasema. Nozibele  
alimpikia mbwa  
chakula.



Kisha mbwa akasema,  
“Nitayarishie kitanda.”  
Nozibele akajibu,  
“Sijawahi  
kumtayarishia mbwa  
kitanda.” “Tayarisha  
au nikuume!” mbwa  
alisema. Nozibele  
alitayarisha kitanda.



Alitakiwa kumpikia,  
kumfagilia na  
kumwoshea mbwa kila  
siku. Kisha siku moja  
mbwa alisema,  
“Nozibele, leo  
nalazimika  
kuwatembelea  
marafiki zangu. Fagia  
nyumba, pika chakula  
na uoshe vitu vyangu  
kabla sijarudi.”



Mbwa alipoenda tu,  
Nozibele alichukua  
nywele tatu kutoka  
kichwani kwake.  
Aliweka mmoja  
mvunguni mwa  
kitanda, mwingine  
nyuma ya mlango, na  
mwingine kwenye zizi  
la ng'ombe.  
Kisha alikimbia  
kwenda nyumbani  
haraka alivyoweza.



Mbwa aliporudi,  
alimtafuta Nozibe.  
“Nozibe, uko wapi?”  
Aliita kwa sauti. “Niko  
hapa mvunguni mwa  
kitanda,” unywele wa  
kwanza ulisema. “Niko  
hapa nyuma ya  
mlango,” unywele wa  
pili ukasema. “Niko  
hapa ndani kwenye  
zizi la ng’ombe,”  
ukasema unywele wa  
tatu.



Papo hapo mbwa  
alifahamu kuwa  
Nozibele alikuwa  
amemdanganya. Kwa  
hivyo, alikimbia moja  
kwa moja hadi kijijini.  
Lakini, ndugu zake  
Nozibele walikuwa  
wamemsubiri kwa  
fimbo kubwa. Mbwa  
aligeuka na kukimbia  
na hadi leo, hajawahi  
kuonekana tena.





